**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**636** **TEHAMA**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A**, na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu wa somo la TEHAMA kufundisha msingi wa ufundishaji unaoweka usawa wa kijinsia darasani.
2. Ainisha faida nne za mkoba wa kazi kama zana ya upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi.
3. Fafanua kwa kifupi aina ya huduma zinazotolewa na UMATI, EMAU, ANGAZA na AMREF – TANZANIA.
4. Eleza faida mbili na kasoro mbili za mwalimu kutumia maswali ya "kweli" na "si kweli" katika mazoezi na mitihani kwa wanafunzi wake.
5. Toa hoja nne za kutetea kuwa mawasiliano kwa njia ya barua pepe ni bora kuliko barua za kawaida.
6. Bainisha mambo manne anayopaswa kufanya mwalimu wa somo la TEHAMA wakati wa kuchambua muhtasari wa somo.
7. Eleza kwa ufupi faida nne za tathmini kama kipengele muhimu katika andalio la somo.
8. Eleza kwa kifupi namna nne zinazoweza kutumika kupanga maandiko katika maktaba kwa kufuata maudhui ya andiko.
9. Tofautisha habari inayotolewa kwa njia ya redio na ile inayotolewa kwa njia ya luninga.
10. Bainisha michoro minne inayochorwa barabarani na ueleze taarifa inayotoa kwa mtumiaji wa barabara.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **Manne** katika sehemu hii.

11. Tathmini mchango wa msingi wa ufundishaji unaompa mwanafunzi uwezo wa kutafuta, kuchambua na kuwasilisha habari na taarifa kwa kutoa hoja tano.
12. Fafanua kwa kina mambo matano yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa kwa kutoa mifano halisi.
13. Jadili kwa hoja tano kwa mifano dhahiri juu ya kauli: "Ili tendo la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA likamilike, mwalimu hana budi kumchunguza mwanafunzi kwa kutumia zana mbalimbali."
14. Eleza uhusiano uliopo kati ya matumizi ya zana na ujifunzaji wa mwanafunzi katika somo la TEHAMA.
15. Jadili hatua sita za kuandaa azimio la kazi katika somo la TEHAMA.
16. Toa maelezo ya kina kuhusu vigezo vitano muhimu vya kuzingatia katika kuchagua na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org